



UYOGAPLUS ENTERPRISE

S.L.P 76321, Dar Es Salaam, info@uyogaplus.com, www.uyogaplus.com



+255765264666



@Uyogaplus



@Uyogaplus

FOMU YA MKULIMA

1.TAARIFA ZA MKULIMA

JINA LA KWANZA..... JINA LA PILI..... JINA LA TATU.....

MAHALIANAPOISHI MAHALI SHAMBA LILIPO

NAMBA YA SIMU NAMBA YA MALIPO

JINA LA AKAUNTI YA BENKI NAMBA YA AKAUNTI.....

2. UTANGULIZI

UYOGAPLUS ni taasisi inayo jihusisha na uzalishaji wa uyoga, mbegu za uyoga, kuuza uyoga pamoja na kutoa elimu ya ujuzi wa kilimo cha uyoga, yenye makao makuu mjini Dar es Salaam. Uyogaplus ina tawi mjini Morogoro, Iringa, Njombe, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro.

3. MALENGO YA UYOGAPLUS

- (a) Kutoa elimu juu ya kilimo cha uyoga kwa watazania wote
- (b) Kuhamasisha ulaji wa uyoga na kukuza soko la uyoga ndani na nje
- (c) Kuuza uyoga uliozalishwa na wakulima wa taasisi
- (d) Kufanya tafiti juu ya uzalishaji wa uyoga pori mbalimbali unaopatikana Tanzania

4. MAJUKUMU YA TAASISI KWA WAKULIMA

- (a) UYOGAPLUS itasambaza mbegu bora za uyoga kwa mkulima pindi anapohitaji, kwa wakati na kwa punguzo la bei la asilimia 50 ambapo mkulima aliejiunga na taasisi ya UYOGAPLUS atanunua mbegu kwa bei ya 1000Tsh@ chupa, badala ya 2000Tsh@ chupa.
- (b) UYOGAPLUS, ni mnunuzi mkuu wa zao la uyoga kutoka kwa wakulima. Bei za uyoga ni kama ifuatavyo Dar es Salaam uyoga mbichi utanunuliwa 7000Tsh@ kilo na mkavu 30,000Tsh@ kilo, mikoa ya Morogoro, Arusha, Dodoma, Kilimanjaro uyoga mbichi ni 6000Tsh@ kilo na mkavu 25,000Tsh@ kilo. Mikoa ya Iringa na njombe Uyoga mbichi ni 5000Tsh@ kilo na mkavu 20000Tsh@ kilo.
- (c) UYOGAPLUS ita kua bega kwa bega katika kutatua matatizo yatakayo jitoza shambani kwa mkulima, ushauri utatolewa kwa njia ya simu una ikibidi mtaalamu atatembelea shamba la mkulima.

5. MAJUKUMU YA MKULIMA

- (a) Mkulima awe na banda lenye vigezo na liwe na uwezo wa kuoteshea mashamba 500 na kuendelea
- (b) Mkulima awe na uwezo wa kuotesha mashamba ya uyoga 3000 au zaidi kwa kipindi cha mwaka mmoja.
- (c) Mkulima atalima uyoga kwa taratibu sahihi za kitaalamu
- (d) Mkulima atanunua mbegu na vifungashio (mifuko ya kupakia kimeng'enywa) kutoka taasisi ya UYOGAPLUS

6. UTARATIBU WA MALIPO

Malipo ya mbegu na vifungashio yatafanyika benki ya **NBC** akaunti namba **040168031046**, Jina la akaunti **JOEL TITO BISOMA**.

Mkulima atawekewa malipo kwenye akaunti yake ya benki kwa malipo yanayo zidi 1,000,000Tsh, malipo chini ya milioni moja yatafanyika kwa njia ya simu. Malipo yatafanyika kwa wiki na kwa mwezi..

7. KUSITISHWA KWA MKATABA

(a) Mkataba huu ni wa mwaka mmoja toka tarehe ya leo hivyo basi mara baada ya kumalizika kwa mda wake kutakua na makubaliano aidha kusitisha au kuingia katika mkataba mpya.

(b) Mkataba utavunjwa pale tu mmoja wa mhusika wa mkataba huu kushindwa kutimiza majukumu yake.

8. SABABU ZA KUSITISHWA KWA MKATABA

Zifuatazo ni sababu za kushindwa kwa mkataba;

(a) Mnunuzi anaposhindwa kumlipa mkulima kwa wakati

(b) Mkulima atakapo tumia mbegu na vifungashio visivyotoka UYOGAPLUS

(c) Mkulima kushindwa kufata taratibu kutoka kwa wataalamu katika uoteshaji, uhudumiaji na uvunaji wa uyoga

(d) Ukeukaji wa kipengele chochote katika mkataba huu.

9. APIZO

Mimi mkulima wa uyoga nimekubaliana na maelezo yote tajwa hapo juu

Sahihi tarehe

MATUMIZI YA OFISI TU

JINA CHEO.....

SAHIHI TAREHE